4. Yahshua alisema nini kuhusu watu wake? Je! watu huweka taa mahali penye giza kwa kusudi gani? Mathayo 5:14, 15 .
5. Je, watu wa Bwana wanapaswa kutumiaje nuru ambayo Elohim amewapa? Mstari wa 16; 2 Wakorintho 4:6.
6. Je! Ni hatari gani inayotishia wale ambao hawaenendi katika nuru? Yohana 12:35.
7. Je! Kanisa la Mitume lilipaswaje kuwa nuru ya ulimwengu? Matendo 1:8.
8. Ni ujumbe gani mkuu unaotolewa kwa kanisa la Elohim? Marko 16:15.
9. Ni ujumbe gani mkuu utakaotolewa kwa ulimwengu wote kabla Yahshua hajarudi? Mathayo 24:14; Ufunuo 14:6-10.
10. Je! Bwana anawaambia nini watu ambao watatoa ujumbe kama huo? Je, matokeo ya kazi ya kumaliza yatakuwa gani? Isaya 60:1-5.

********************************

**Somo la 4 Juni, 2022 (Sivan 5, 5782).**

## URITHI ULIO HAKIKISHWA

**Somo Kuu: 2 Petro sura ya 2.**
**Fungu La Kukariri: Phil. 3:14.**

1. Je! Ni hatua gani ambazo ni muhimu katika kuutafuta uzima wa milele? Waebr. 11: 6; Matendo 3:19; Wagal. 3:27.



6. Baba wetu wa mbinguni ako tayari kutupea uwezo kutoka juu kama vile tuko tayari kutoa chakula kwa watoto wetu wakati wako njaa? Luka 11:11-13.

   **Maelezo**: Roho hii takatifu iliyonenwa pia kama Roho Mtakatifu, kama "wema", na "nguvu". Ni sehemu ya Baba mwenyewe, uweza kutoka mbinguni huja katika hekalu zetu na inatufanya tuwe wenye roho. Hutujaza wema, na hutujaza kwetu sifa za Mbinguni ambazo Masihi Mwokozi wetu alipambwa kimiujiza. Ni kupitia kupokea uwezo huu katika miili yetu tu, huwa tunajazwa haki.
7. Ni muhimu kwetu kuwa na njaa kwa ajili ya, na kuwa na hamu ya nguvu hii ambayo itatufanya kuwa wenye haki? Mathayo 5:6.

   **Maelezo**: Watu wengi, kwa wakati huu, huwa na njaa na kiu ya vitu vya dunia hii, umaarufu, nafasi, pesa na anasa, ambayo yote ni ubatili, na karibuni hayo yote yatapita mbali.
8. Ni nani ambaye alifungua njia, na alitufundisha kuhusu sheria hii kwa ajili ya Roho ya uzima wa milele? Yohana 8:12.
9. Je, Mwokozi wetu ambaye alikuja kutuonyesha njia, mara kwa mara alitumia muda kukawia mbele ya baba yake, katika maombi? Luka 6:12.



3. Zawadi ya wasioamini ni nini? Mathayo 25: 28-30.
4. Je, Bwana ni mwaminifu kwetu? Zaburi 119:90; Zaburi 143:1; Maombolezo 3:23.
5. Je, tunaweza kujifunza nini kupitia kujaribiwa kwa imani yetu? Yakobo 1:3.
6. Je, tuna uwezo wa kufanya miujiza kwa sheria au ni kwa imani? Wagalatia 3:5; Matendo 6:8.
7. Tunafaa kutosheleka na imani yetu katika Bwana, au lazima tutatafuta kuwa na matendo pia? Yakobo 2:14, 19, 22.
8. Tutahesabiwa haki kwa matendo au imani pekee yake, au tunafaa kuwa na imani na matendo? Wagalatia 2:16; Yakobo 2:21-24.
9. Tuna haja ya kuonyesha tu imani yetu au lazima tuonyeshe imani yetu kwa matendo yetu? Yakobo 2:18, 26.

********************************



***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Pili
2022

Ya
Aprili, Mei, Juni.
**(Nisan, Iyar, Sivan)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568, Jerusalem — Israel**

10. Baada ya kukaa usiku katika maombi, ni nini ilitoka kwake na kuingia katika watu ambao waliponywa? Luka 6:19.

**Maelezo**: Wengi wetu walicheza na sumaku wakati walikuwa watoto, au kipande cha chuma kupata nguvu kutokana na sumaku ya umeme, na kuangalia jinsi itachukua vipande vidogo vya chuma, na kuvishikilia kwa nguvu. Tunaweza kuvuta hizo kwa mara nyingi na kuiacha izivute tena na tena. Kwa muda mchache hii chuma pia itapata hizo nguvu za sumaku, mpaka itavuta vipande vidogo pia. Hii inaonyesha jinsi mtu hutumia muda wake katika maombi ya kila siku anaongezeka nguvu kutokana na nguvu na wema wa mbinguni, ambapo dhambi zinaondolewa kutoka kwa miili yetu, na inakuwa hekalu kwa ajili ya Roho Mtakatifu kupata nafasi ya kuishi.

11. Baada ya Bwana kutumia muda wake katika maombi, nini kilichotokea kwa mwanamke ambaye aliliguza pindo la vazi lake? Luka 8:43-47.

*******************************



11. Je! Ni ugonjwa gani ambao Yahshua aliongea kuhusu? Mstari wa 13 (sehemu ya mwisho).
12. Je! Mmoja wa wanafunzi wa Yohana alimwuliza swali gani? Mstari wa 14.
13. Yahshua alimpa maelezo gani? Mathayo 9:15.
14. Alitumia mfano gani kumjibu? Mstari wa 16, 17.
15. Yahshua aliombwa ombi gani wakati huo? Mathayo 9:18.
16. Yahshua alifanya nini? Mstari wa 19, 24, 25.

**Maelezo**. Masihi anaweza na kila wakati yuko tayari kuwasaidia wale wanaomwamini, wawe watenda dhambi au watakatifu. Anajali kuhusu magonjwa na shida zetu. Hebu tuweke imani yetu kwake.

*******************************

**Somo La Mei 21, 2022 (Iyar 27, 5782).**

## WACHA NURU INGAZE

**Somo Kuu: 1Wathesalonike 5.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 8:12.**

1. Nuru ya ulimwengu ni nani? Wataenendaje wale waifuatao nuru? Yohana 8:12; 9:5.
2. Je! Yahshua aliachaje nuru yake iangaze? Matendo 10:38.
3. Ni nini imenenwa kuhusu miji aliyoitembelea? Mathayo 4:16.



**Somo La 2 Aprili, 2022 (Nisan 1, 5782).**

## KUITWA KWA KAZI MAALUM KWA WAKATI MAALUM

**Somo Kuu: Ufunuo sura ya 16.**
**Fungu La Kukariri: Ufunuo 16: 1.**

1. Ni juu ya nani ambaye pigo la kwanza kati ya yale mapigo saba ya mwisho lilimwagiwa? Ufunuo 14:9, 18: 4.
2. Ni ishara gani mbili zimepeanwa kwa wakati huu maalum wa maandalizi? Nahumu 2:3.
3. Kumekuwa na jumbe tatu kwa dunia yote, ambazo zilitumwa tangu mwanzo wa injili. Ni nini na ni wakati upi ujumbe wa kwanza ulitolewa? Ufunuo 14: 6.

**Maelezo**: Huu ulikuwa ujumbe uliotumwa mbele katika siku za Mitume, katika ulimwengu wa waabuduo sanamu ili kuharibu sanamu zao na kumwabudu yeye aliyeziumba mbingu na dunia. Ilikuwa pia saa ya hukumu juu ya taifa la Wayahudi (Luka 21:24), na juu ya mkuu wa ulimwengu huu.

4. Ni nini imesemwa kuhusu wakati wa hukumu ambayo ilikuwa sehemu ya ujumbe wa kwanza kwa dunia yote? 1 Petro 4:17; Yohana 16:7-11; 12:31.



10. Licha ya kuonyesha wenye dhambi kuhusu makosa ya njia zao, na kuwavuta wao kwa ufalme, ni kazi gani nyingine tumepewa kufanya? Mithali 19:17; Isaya 1:17.
11. Ni nini kilichosemwa kuhusu wale ambao wataziba masikio yao wasisikie kilio cha maskini? Mithali 21:13.
12. Ni nini imetangazwa kuwa dini iliyo safi? Yakobo 1:27.

*******************************

**Somo La Juni 25, 2022 (Iyar 26, 5782).**

## IMANI NA MATENDO

**Somo Kuu: Waebrania 11:1-13**
**Fungu La Kukariri: Wagalatia 3:9**

**Maelezo**: WaMasihi wengi leo wameuliza swali, ni kwa imani au ni kwa matendo yetu kwamba huwa tunaokolewa? Somo la leo linaonyesha kwamba imani haipaswi kuwa bila matendo wala matendo kuwa bila imani. Lakini tusichanganye matendo au imani na neema ya milele ya Baba ambayo huwa tunapata tu kupitia Mwanawe wa pekee.

1. Tunapaswa kufanyia nini talanta ambazo Elohim anatupatia? Mathayo 25: 15, 16.
2. Zawadi ya waumini ni nini? Mathayo 25:21.

**Somo La Mei 21, 2022 (Iyar 20, 5782).**

## KUPONYA KIWETE; KUITWA KWA MATHAYO

**Somo Kuu: Mathayo 9:1-12.**
**Fungu la Kukariri: Mathayo 9:12.**

1. Je! Yahshua alienda wapi? Mathayo 9:1.
2. Ni nani aliletwa kwake kwa ajili ya uponyaji? Badala ya kumponya, Yahshua alimwambia nini? Mathayo 9:2.
3. Je! Aliletwa kwa Yahshua katika hali gani? Marko 2:1-5.
4. Waandishi walifikiri nini juu ya Yahshua kwa sababu alimsamehe dhambi huyo mtu? Marko 2:6, 7; Mathayo 9:3.
5. Je! Yahshua aliwaambia nini kuhusu mamlaka yake ya kusamehe dhambi? Mathayo 9:4-6.
6. Je, umati ulichukuliaje uponyaji huu? Mathayo 9:7, 8; Marko 2:12.
7. Je! Yahshua aliwaita nani wawe wafuasi wake? Mathayo 9:9; Marko 2:14.
8. Je! Yahshua aliketi kula chakula katika nyumba ya nani? Ni nani ambaye aliketi pamoja Naye? Marko 2:15; Mathayo 9:10.
9. Je! Wafarisayo walitoa shutuma gani kwa sababu ya jambo hilo? Mathayo 9:11.
10. Je! Yahshua alijibuje kwa ajili ya pingamizi hili? Mathayo 9:12.



**Somo La Aprili 23, 2022 (Nisan 22, 5782).**
**TABIA NA MADHUMUNI YA MAISHA**

**Somo Kuu: Wafilipi sura ya 4.**
**Fungu La Kukariri: Wafilipi 4:7**

1. Je, ni tabia gani ya ubinafsi itakuwa dhahiri miongoni mwa watu katika siku za mwisho? 2 Timotheo 3:1-5.
2. Je, mabaki ya Kanisa wanafaa kujipenda wenyewe, na kutafuta utukufu wa bure? Wafilipi 2:3.
3. Je, tunapaswa kujishughulisha na mambo yetu wenyewe pekee? Wafilipi 2:4.
4. Nia kama uwezo unaotuongoza, ni maagizo gani tumepewa kuhusu nia zetu? Wafilipi 2:5; Warumi 12:2.
5. Yahshua alijaribu kujitafutia sifa yake mwenyewe? Wafilipi 2:7.
6. Je, nia ya Yahshua ilimuongoza katika njia ya kujitoa kama sadaka, au ni katika faraja, heshima na anasa? Wafilipi 2:8.
7. Ingawa hakuwa hakitafuta furaha, faraja, au heshima, lakini baada ya kupitia njia ya huzuni na udhalilishaji, hali yake ya mwisho ilikuwa ipi? Wafilipi 2:9.
8. Ni nini ilifanya kazi ndani yake katika kutimiza utukufu huu wa mwisho? Wafilipi 2:13.



2. Ni kitu gani kingine kimetolewa kwa wanafunzi wake? Mathayo 25: 15.
3. Kwa hivyo wanafunzi pia huitwa vipi, ambao wamepewa kazi? Mathayo 25: 14.
4. Ni nini kinatokea kwa kila mmoja ambaye anashindwa katika usimamizi wake kuleta nyongesa kwa ufalme? Yohana 15:2.
5. Ni muhimu kuwa na uhusiano wowote maalum na mbinguni, kwa ajili ya uwepo wa kudumu kwa Roho? Yohana 15:4, 5.
6. Je, ni mahitaji gani maalum tunahitaji ili maombi yetu yasikike na yajibiwe? Yohana 15:16.
7. Ni nini kitatokea kwa wanafunzi wote ambao wanaishi tu kwa nguvu zao wenyewe na hawakai daima katika Masihi? Yohana 15:6.

   **Maelezo**: Nguvu ya injili ambayo huleta uthibitisho kwenye moyo wa mwenye dhambi, na inatoa ushindi kwa mtumishi juu yake mwenyewe, inapeanwa tu kupitia mawasiliano ya mara kwa mara na Mwokozi kupitia kwa maombi. Kuacha kuomba ni kama kutoa waya ya jenereta kwenye gari lako. Nuru yako itapungua hivi karibuni, na hatimaye kuzimika.

8. Ahadi gani imetolewa kwa wale watapanda mbegu ya injili? Zaburi 126:5, 6
9. Je! Ni ahadi gani imepeanwa kwa yule atakayevuta roho za watu? Mithali 11:30; Danieli 12:3.



5. Je! Asili ya ujumbe wa malaika wa pili ni nini? Ufunuo 14: 8.
6. Je! Asili ya ujumbe wa malaika wa tatu ni nini, na ni juu ya nani hasa umeelekezwa? Ufunuo14:9, 10.
7. Je, ni tukio gani linalofuata ujumbe huu? Kuna ujumbe mwingine bado utapeanwa, au ni wakati wa mfalme kuja na kutawala? Ufunuo 14:14-16.
8. Je, Ufunuo 15:1 pia inatuambia nini kuhusu mapigo haya ya mwisho?

   **Maelezo**: Ujumbe wa kumtambua mnyama, na kutoa tahadhari hii, ni "chakula cha wakati unaofaa". Ni ujumbe huu ambao umefika wakati wake katika ulimwengu kwa wakati huu maalum.

*******************************

**Somo la Aprili 9, 2022 (Nisan 8, 5782).**

## CHAKULA CHA JIONI CHA BWANA

**Somo Kuu: Yohana 6: 22-71.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 6:54.**

1. Yahshua alienda wapi baada ya kuwalisha watu elfu tano? Yohana 6: 24, 25.

9. Tunafaa kupokea kwa furaha mateso katika maisha au tunafaa kunung'unika dhidi ya hatima yetu? Wafilipi 2:14.
10. Jinsi gani ni lazima tuenende, na ni kwa madhumuni gani Elohim ametuweka duniani? Wafilipi 2:15.
11. Jinsi gani tutaweza kupata nguvu na kuwa na nia kama ya Masihi? Mathayo 7:7, 8.
12. Baada ya kupokea Roho Mtakatifu wa kumpa uwezo kwa ajili ya huduma, alitupea maagizo yanayohusu kupokea Roho Mtakatifu? Luka 11:11-13.
13. Ni nini tunafaa kusahau, na ni kwa ajili ya nini tunafaa kukaza mwendo kufikia? Wafilipi 3:13, 14.

********************************

**Somo la Aprili 30, 2022 (Nisan 29, 5782).**

## KUENENDA NA KUDUMU KATIKA HAKI

**Somo Kuu: Wakol. Sura ya 3.**
**Fungu La Kukariri: Kol 3:23.**

1. Baada ya kupokelewa katika familia ya Mbinguni, tunapaswa kutafuta nini kila wakati? Wakol. 3:1.
2. Tunapaswa kufikiria jinsi gani kuhusu wakati uliopita, na tunapaswa kupanga jinsi gani kwa ajili ya wakati ujao? Mstari wa 2 na 3.



6. Wakati mtu anapokea "Maji ya uzima", mahitaji yake ya ndani yatakuwa yametimilizwa? Yohana 4:13, 14; 6: 35.
7. Katika tukio tofauti ni mwaliko gani uliweza kumfikia kila mtu? Yohana 7:37-39.
8. Jinsi gani Yahshua alifafanua kuhusu Maji ya uzima? Yohana 7:39.
9. Wakati tunapojazwa na Roho, jinsi gani tutakavyoenenda? Wagalatia 5:16, 25, 26; Warumi 6:11-13.
10. Je! Tunda gani la utakatifu litadhihirika wazi katika maisha yetu ikiwa tutajisalimisha kwa Mwokozi kabisa? Waefeso 5:9, 10; Wagalatia 5:22, 23.

**Maelezo**: Wengi leo hawajakubali kujitolea kwa Bwana kabisa na hawana furaha iliyo yakuwatosheleza kwa kina katika maisha yao ya uMasihi. Kumtumikia Masihi, kwao, ni mzigo badala ya furaha. Kama wewe haujajitolea kwa yote kwake Bwana — fanya hivyo leo!

********************************



2. Kwa nini umati ulikuwa ukimtafuta? Yohana 6:26
3. Yahshua aliwaambia nini kuhusu chakula? Alisema ni wapi chakula hiki kitapatikana? Yohana 6:27
4. Je! Inaonekana kana kwamba umati wa watu walidhani wanao mkate huu kutoka mbinguni? Yahshua alijibuje? Yohana 6: 31-35.
5. Je! Wayahudi walijibu vipi kuhusu taarifa hii ambayo Yahshua alitoa? Yohana 6:42.
6. Je! Yahshua alijibu vipi kuhusu kunung'unika kwao? Yohana 6: 48-51, 53-58.
7. Yahshua alipoanzisha Chakula cha Bwana chaa jioni, alisema mkate usiotiwa chachu uliwakilisha nini? Luka 22:19; Mathayo 26:26. Linganisha na Yohana 6: 51, 53.

**Maelezo**: Wakati Yahshua na wanafunzi wake walikuwa wakila Pasaka, Yahshua alichukua mkate, akaubariki na akasema, chukua, kula, huu ni Mwili Wangu. Mkate huu usiotiwa chachu uliwakilisha Mwili wake. Kula Mwana-Kondoo wa Pasaka sasa ilikuwa jambo lilopita milele. Pasaka ya Agano la kale ilifanywa kuwa historia; Yahshua alikuwa akianzisha Chakula cha jioni cha Bwana.

8. Baada ya kula mkate usiotiwa chachu, Yahshua alifanya nini? Luka 22: 20; Mathayo 26:27.



7. Je! Tutafanya kazi lini? Mhubiri 11:6.
8. Je, wale wanaofanya kazi katika hali ya hewa nzuri tu wana ahadi ya mavuno mazuri? Mhubiri 11:4.
9. Ni kwa nini tunapaswa kushiriki katika kazi hii kubwa bila kukawia? Yohana 9:4.
10. Je, kila moyo unapaswa kujaa huruma na upendo kwa wale ambao wanafanya kazi kwa ajili yao? Zaburi 126:5,6.
11. Ni ahadi gani kubwa inayotolewa kwa wale wanaogeuza watu kwa utakatifu? Danieli 12:3.
12. Sisi tukiwa wanafunzi wa Masihi tutaweza kuthibitishaje kwamba sisi ni wanafunzi? Yohana 15:8.
13. Ni kweli gani mbili za ajabu tunapaswa kuelewa tunapofanya kazi katika shamba Lake la mizabibu? Isaya 55:10-11; 1 Wakorintho 13:8.

********************************

**Somo La Juni 18 2022 (Iyar 19, 5782).**

## MABAKI YA WAUMINI WANA KAZI YA KUFANYA

**Somo Kuu: Yohana 15**
**Fungu La Kukariri: Yohana 15:8**

1. Kila mtumishi mwaminifu amepewa kitu cha kufanya? Marko 13:34.

Baadhi yetu huweka hazina ya uovu, wivu, hasira, na udanganyifu katika nafsi zetu na kukataa kuviuza vyote ili kununua lulu ya thamani kuu, lulu ambayo ni Masihi na ufalme.
*******************************

**Somo La Mei 14, 2022 (Iyar 13, 5782).**

## MAJI YA UZIMA

**Somo Kuu: Isaya 12**
**Fungu La Kukariri: Ufunuo 22:17.**

1. Je! Mwaliko wa Elohim kwa wote wenye kiu ni upi? Isaya 44: 3; 55: 1.
2. Ni kwa njia gani tutateka maji kutoka visima vya wokovu? Isaya 12: 2, 3.
3. Je! Yahshua alifanya ombi gani rahisi kwa yule mwanamke katika kisima cha Yakobo? Yohana 4: 6, 7.
4. Jibu lake mwanamke lilikuwa lipi? Yohana 4:9.
5. Jinsi gani mwanamke alijibu wakati Yahshua alimwambia kuhusu maji ya uzima? Yohana 4:10-12.

**Maelezo**: Ni dhahiri kutokana na jibu la mwanamke huyo kwamba hakuelewa kile Mwalimu alimwambia - alifikiria tu maji ya muda.



3. Je! Tunafaa kuondoa mambo gani? Mistari ya 5-8.
4. Tunapaswa kuvaa nini? Mstari wa 10 na 11.

**Maelezo**. Ona kwamba mambo ya awali yote yalikuwa ni vyombo vya kifo, kwa sababu yanatoka katika moyo mbaya na yanahusiana na maneno na matendo yetu. Tunapovaa utu upya, tunaanza kujenga maisha ya milele.

5. Utu upya unalishwaje? Mstari wa 16.
6. Je! Maneno na matendo yetu yanayotoka moyoni yanapaswa kuwa nini hasa? Mstari wa 14.
7. Tunapaswa kutegemea nini kila siku ili kuongoza maneno na matendo yetu? Mstari wa 17.
8. Baada ya kuchagua njia hii iliyo sawa, na kujitayarisha kikamilifu kutembelea juu yake, je, tunapaswa kufanya kazi shingo upande au ni kwa kuwafurahisha wanadamu? Mstari wa 23.
9. Je! Ikiwa matendo yetu hayafai, kazi yetu au mahali petu miongoni mwa mabaki itakuwaje? Warumi. 1:18.
10. Je, wote wanaoamini wanapaswa kuwa na uwezo wa kutosha wa kuishi maisha matakatifu? Mstari wa 16 na 17.
11. Tukimwomba kwa imani, Bwana atatufanyia nini? 1 Thes. 3:12, 13 .
12. Je! Ni nini thawabu yetu ya hakika ikiwa tutaongezeka na kuzidi katika upendo, saburi,



12. Tunapojitahidi kushinda ulimwengu huu na tamaa za kimwili, ni nini tunaagizwa kufanya kila mara? Waefeso. 6:18.
*******************************

**Somo La Juni 11 2022 (Iyar 12, 5782).**

## KAZI ILIYO NA UTUKUFU NA THAWABU

**Somo Kuu: 1 Wakorintho 15:41-58.**
**Fungu La Kukariri: 1 Wakorintho 15:28.**

1. Je! Tunapaswa kuvumilia nini tukiwa askari wa Masihi Yahshua? Luka 21:16,17.
2. Je! Watenda kazi wa Bwana wanapaswa kuvikwa nini? Waefeso 6:10-18.
3. Je! Shamba la Bwana ni lipi (ambalo kila mshirika wa kanisa ni mtenda kazi)? Mathayo 13:38.
4. Je! Tunapaswa kutumia nini katika kazi ya Bwana? Marko 4:14.
5. Ni wapi katika shamba hili kuu? Tutafanya wapi kazi hii yote muhimu? Mhubiri 11:1, 2; Luka 14:21, 23 .
6. Ni mfano gani wa kufanya kazi ambao umetolewa kwetu kama ulivyoonyeshwa na Bwana na mitume kuhusu kufanya kazi nyumba kwa nyumba? Luka 5:29-32; 7:36; 19:1-5; Matendo 20:20.



9. Je! Yahshua alisema kwamba kinywaji kilichokuwa kwenye kikombe kiliwakilisha nini? Mathayo 26:28; Luka 22:20. Linganisha na Yohana 6: 53,54.
10. Kikombe ambacho Yahshua aliwapatia wanafunzi wake kilikuwa na nini? Marko 14:25; Mathayo 26:29.

**Maelezo**: Injili za Marko, Luka na Yohana, zinatuambia kwamba kikombe ambacho Yahshua alibariki kilikuwa na matunda ya mzabibu. Hii ilikuwa damu safi ya zabibu, ambayo inawakilisha Damu ya Yahshua iliyo ya thamani. Tazama Kumbukumbu la Torati 32:14, sehemu ya mwisho.

11. Je! Neno Ushirika linafaa kutumiwa kumaanisha chakula cha jioni cha Bwana katika maandiko? 1 Wakorintho 10:16.
12. Je! Yudasi alikuwepo na alishiriki chakula cha jioni? Luka 22:21; Yohana 13:18.
13. Je! Kila nafsi inapaswa kufanya nini kabla ya kula chakula cha jioni cha Bwana? Ikiwa tutashindwa, matokeo ya kusikitisha yatakuwa nini? 1 Wakorintho 11: 27-30.
*******************************

kutii, kama watumishi wenye faida? 1 Thes. 4:1, 16, 17; 1 Wakor. 15:58.

**Maelezo**. — Watu wa ulimwengu wanapendezwa tu na kazi zao wenyewe na faida zao wenyewe, lakini sivyo ilivyo kwa mtu anayetafuta uzima wa milele. Mtu huyo, awe mzee au kijana, atakuwa na sehemu kubwa katika kazi ya Bwana. Kazi yake mwenyewe katika taaluma yake itakuwa ya pili katika maisha yake, na "Kazi ya Ufalme" itakuja ya kwanza na itasaidiwa kwa kujitolea na sehemu ya mapato yake, ambayo inawakilisha sehemu ya maisha yake.

*******************************

**Somo la Mei 7, 2022 (Iyar 6, 5782).**

## UKAMILIFU KATIKA NJIA YA UZIMA

**Somo Kuu: Wafilipi 3.**
**Fungu La Kukariri: Wafilipi 3:14.**

1. Je! Nuhu alifikia kiwango kipi katika siku alizoishi? Mwanzo 6:8, 9.
2. Je! Ni kiwango gani Elohim alihitaji kutoka kwa Ibrahimu? Mwanzo 17:1.
3. Je! Ni nini inayoonyesha kwamba Henoko aliufikia ukamilifu? Mwanzo 5:22-25; Waebrania 11:5.



4. Je, agano jipya inasema nini kuhusu Zakaria na Elisabeti? Luka 1:5, 6.
5. Ni katika hali gani Elohim aliahidi kuimarisha Sulemani juu ya kiti cha enzi cha mfalme Daudi? 1 Wafalme 9:3-5.
6. Je! Nini kilichosemwa kuhusu wale walioufikia ukamilifu? Zaburi 37: 37..
7. Ni maagizo yapi yaliotolewa kwa Israeli kwa ajili ya huu utimilifu? Kumbukumbu la Torati 18:9-13.
8. Ni nini kilichosemwa kuhusu mataifa ya Kanaani? Kumbukumbu la Torati 18:14.

**Maelezo**: Katika pembeni mwa Bibilia inaonyesha "kamili" kama "unyofu" au "uaminifu". Mtu mkamilifu ni yule aliye mwaminifu na hana nia ya kufanya makosa.

9. Ni nani ambaye Bwana wetu Yahshua alimweka kama mfano kwetu wa ukamilifu? Mathayo 5:48.
10. Je! Matajiri wanafaa kufanya nini ili waweze kuufikia ukamilifu? Mathayo 19:16-21.
11. Jinsi gani tajiri yule alijibu kuhusu hitaji hili? Mathayo 19:22.
12. Katika fumbo fulani, ni kiasi gani tunatakiwa kuuza ili kupokea wokovu? Mathayo 13:45, 46.

**Maelezo**: Ubinafsi ndio kikwazo pekee katika lengo letu la kuufikia ukamilifu. Tunaviuza vyote?



**Somo la Aprili 16, 2022 (Nisan 15, 5782).**

**KUONGEZEA NGUVU SUMAKU YA BINADAMU KUTOKANA NA NGUVU ZA USHINDI**

**Somo Kuu: Warumi 8:1-14.**
**Fungu La Kukariri: Warumi 8:28.**

1. Kuna sheria inayoongoza Roho katika utendaji wa kazi ndani ya miili yetu? Warumi 8:2.
2. Hii sheria ya Roho ya uzima itafanya nini ndani yetu kulingana na sheria? Warumi 8:2.

**Maelezo**: Wakati sheria hii takatifu ya Roho inaruhusiwa kufanya kazi ndani yetu, kwa asili tutazaa matunda ya Roho, na kwa hivyo tutaenenda katika kwa kutii kamili amri zote. Hivyo basi tutakuwa huru kutokana na hukumu ya sheria hii, ambayo huleta mauti.

3. Kuna mahali maalum mwilini mwa kila mtu, kwa ajili ya kuishi kwa Roho Mtakatifu? 1 Wakorintho 3:16 na pia 1 Wakorintho 6:19, 20.
4. Kama miili yetu haina nguvu ya hii Roho, na kwa hivyo kuwa najisi kwa sababu ya uwepo wa roho ovu, tamaa za kidunia, hisia, na dhambi, matokeo ni nini? 1 Wakorintho 3:17.
5. Ili sisi tupokee Roho hii, tunahitaji kufanya hatua ya kwanza, au tutasubiri Elohim kuingia ndani yetu? Yakobo 4:8-10.



2. Ni tuzo gani kubwa tunapaswa kutafuta kwa bidii? Wafilipi 3:14.
3. Ili kujihakikishia uteuzi wetu, ni tahadhari gani na ushauri maalum unaotolewa? 2 Petro 1:10.
4. Kwa maisha ya bidii na huduma ya faida kwa Bwana, tunakubaliwa kuingia katika ufalme gani, na ni nini hali ya uvumulivu wa uraia wake? 2 Petro 1:11.
5. Baada ya kupokelewa kama watahiniwa wa urithi huu, ni wapi tunapaswa kuweka ari yetu? Wakolosai. 3: 1, 2.
6. Tunapaswa kutafakari nini na kuifanyia kazi kwa bidii? Wafilipi 3:20.
7. Nia ya Masihi ilikuwa imejaa mawazo ya kazi ya kuhubiri injili; na kama mfanyakazi wa wito wa mbinguni alifaidika, tunapaswa kuwa na nia gani? Wafilipi 2: 5.
8. Ili nia zetu ziwe juu ya mambo yaliyomhusu Masihi zaidi, je ni muhimu kwetu kujifunza maisha na kazi zake? Wafilipi 3: 8, sehemu ya kwanza; 2 Petro 3:18.
9. Ili tuweze kuyafikia yaliyo juu ambayo tunayatamani, ni nini tunahitaji kujua? Wafilipi 3:10, 11.
10. Tunapaswa kusahau nini, na tunapaswa kuyafikia mambo gani yaliyo mbele? Wafilipi 3:13.
11. Kama tunapoendelea kukaza mwendo ni nini tunaagizwa kuweka mbali, na ni nini tunachoambiwa tukitamani? 1 Petro 2: 1, 2.